



TANGAZO KWA

UMMA

**MWALIKO WA KUSHIRIKI MAONESHU YA 44 YA BIASHARA YA KIMATAIFA
YA DAR ES SALAAM (DITF) YATAKAYOANZA TAREHE 28 JUNI HADI 13
JULAI, 2020**

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) inapenda kukaribisha Taasisi za Umma na Sekta Binafsi pamoja na Jumuiya ya Wafanyabiashara kutoka Ndani na Nje ya Tanzania kushiriki katika Maonesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayotarijiwa kufanyika tarehe 28 Juni hadi 13 Julai, 2020 katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl J.K.Nyerere, barabara ya Kilwa Dar es Salaam.

Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yamesajiliwa na kutambulika na Taasisi ya Umoja wa Maonesho Duniani (UFI) na kama Maonesho bora katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Maonesho haya ni jukwaa la kipekee la Kimataifa la kutoa huduma ya ukuzaji wa huduma na biashara ndani na nje ya nchi.

Kwa Mwaka 2019, Maonesho ya DITF yalivutia waoneshaji kutoka nchi 35 duniani ambapo 520 kutoka Nje ya Nchi, 3250 kutoka ndani ya Tanzania na watembeleaji zaidi ya 700,000. Maonesho ya 44 ya DITF yatatoa pia fursa ya mikutano ya kibiashara ya Ana kwa Ana (*B2B Meetings*). Huduma ya Kliniki ya Biashara (*Business Clinic*) na matukio mbalimbali ya kisekta kupitia siku maalum.

Ili kushiriki Maonesho haya tafadhali pakua fomu kupitia tovuti yetu yenye anuani www.tantrade.go.tz au tembelea ofisi za TanTrade zilizopo katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl J.K.Nyerere, barabara ya Kilwa Dar es Salaam. Wasilisha maombi yako kabla ya tarehe 31 Machi, 2020. Tafadhali malipo yakamilishwe yote wakati wa uwasilishwaji wa maombi.

Kwa taarifa zaidi unaweza kuwasiliana nasi kwa barua pepe: sac@tantrade.go.tz au simu namba +255 754 265 822

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu,

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade),

S.L.P 5402

DAR ES SALAAM.